OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA
SHULE YA SEKONDARI NKOMA DAY
S.L.P 349- ITILIMA-SIMIYU- 0756095406/0621632076

JINA LA MWANAFUNZI .....

1.0 Ninafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Nkoma day, shule hii ipo katika kata ya Nkoma kijiji cha Nkoma

2.0 Shule inamchepuo wa sanaa na sayansi inafundisha masomo ya **Civics, History, Geography, Kiswahili, Basic Mathematics, Chemistry, Biology, English na Physics**

3.0 Masomo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipouwa soma la Kiswahili

4.0 Muhula wa kwanza utaanza tarehe 11,January,2021, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo.

MAMBO YA KUZINGATIA

SARE ZA SHULE

A. **WAVULANA**

1.0 *suruali mbili kitambaa moja rangi ya kaki na nyingine rangi ya damu yam zee (maroon), zenye marinda ya* mikunjo ya juu (turn up)

2.0 atakaye shona suruali isiyokuwa na maadili na chini ya kiwango kinachotakiwa hataruhusiwa kuvaa shuleni

3.0 shart jeupe (nyeupe), mikono mifupi ,soksi jozi mbili rangi nyeusi

4.0 viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili zenye kamba kamba na visiwe na kisigino kirefu

5.0 mkanda wa suruali mweusi belt ndogo, vifaa vya michezo traki rangi nyeusi na fulana rangi ya blue za mazoezi na shughuli za elimu ya kujitegemea (EK) zinapatikana madukani.

6.0 Sweta rangi ya bluu,(zinapatikana madukani)

7.0 Daftari kubwa kumi (10 counter books), mathematical set moja, dictionary ya kiingereza moja na kamusi ya kiswahili

B. **WASICHANA**

1.0 Sketi mbili rangi ya kitambaa moja kaki na nyingine rangi ya damu ya mzee zenye rinda kubwa kubwa, atakayeshona sketi isiyokuwa na maadili na chini ya kiwango kinachotakiwa hataruhusiwa kuivaa shuleni

2.0 Shart jeupe (nyeupe), mikono mifupi, soksi jozi mbili rangi nyeupe zisizo na mapambo ya aina yoyote.

3.0 Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili na visiwe na kisigino kirefu

4.0 Sweta la rangi ya bluu (zinapatikana madukani), vifaa vya michezo traki rangi nyeusi na Fulana za rangi ya bluu za mazoezi na elimu ya kujitegemea (EK), zinapatikana madukani

5.0 Daftari kubwa kumi (10 counter books), mathematical set moja, dictionary ya kiingereza moja na kamusi ya Kiswahili

C. **KWA WANAFUNZI WOTE**:

NB: vazi la hijabu (kwa wale waislamu wasichana), ifanane na sare ya shule

.Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu ambazo zitajazwa kikamilifu na kuzikabidhi wakati wa kusajiliwa shuleni

.Kwa Yule aliye na matatatizo ya kiafya aje na cheti cha daktari kwa udhibitisho ili atambulike shuleni

.Sheria na kanuni za shule zisomwe na kuzingatiwa kwa kila mwanafunzi

HONGERA SANA/KARIBU SHULE YA SEKONDARI NKOMA DAY

Blatoma.
.....

THE HEADMISTRESS
NKOMA SEC SCHOOL
P.U. Box 349
BARIADI

SHULE YA SEKONDARI NKOMA DAY
S.L.P 349 BARIADI - SIMIYU

SHERIA, KANUNI NA TAARIFA ZA SHULE.

A. SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuepuka kabisa makosa yafuatayo;-

Haya yanaweza kukusababishia ufukuzwe shule kwa mujibu wa sheria ya Wizara ya Elimu sayansi teknolojia na Mafunzo ya Ufundi

- Wizi wa aina yoyote
- Ugomvi, lugha chafu na kupigana
- Udanganyifu katika mitihani ya aina yoyote
- Kujaribu kusababisha au kuongeza na kushiriki kugoma kwa mwanafunzi
- Ubakaji
- Uasherati pamoja na kupatikana na vifaa vya aina hiyo
- Ulevi wa aina yoyote
- Uvutaji sigara, Bhangi na madawa ya kulevya
- Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
- Kupata au kusababisha mimba
- Kutoa mimba
- Kukataa adhabu kwa makusudi
- Kudharau Bendera na wimbo wa Taifa
- Utoro

B. KANUNI MUHIMU ZA SHULE

1. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni saa 1:00 asubuhi na kuondoka kwa muda uliopangwa
2. Mwanafunzi anapaswa kuwa mtii mwenye adabu na mnyenyekevu nyakati zote na popote zaidi ya yote awe na nidhamu ya hali ya juu
3. Mwanafunzi akiwa nje ya darasa asimame na kusalimia kwa heshima na adabu kwa walimu na wanafunzi au mgeni yeyote atakayetembelea shule
4. Ni marufuku kuonesha au kujaribu kuonesha mahusianao ya kimapenzi, wanafunzi wote ni watoto wa familia moja.
5. Ni lazima kila mwanafunzi avae sare sahihi za shule wakati wote wa nyakati za shule
6. Ni marufuku mwanafunzi kuonekana kwenye vilabu vya pombe , bar, kumbi za starehe na majumba ya kulala wageni (Guest house) na kucheza pool table
7. Ni marufuku kuvaa pete, hereni, kofia, kufuga nywele ndefu na ndevu, kucha ndefu, rangi ya vidole (kucha) na mdomo pamoja na kutochomekea shati
8. Ni marufuku mwanafunzi kuongea lugha zisizo rasmi shuleni. Kiingereza ndio lugha ya pekee ya mawasiliano wakati wote wa shule
9. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni
10. Ni lazima kila mwanafunzi aoneshe bidii kubwa katika masomo darasani pamoja na mitihani ya mara kwa mara inayotolewa na shule kuacha kufanya mitihani pasipo sababu ya msingi ni **KOSA KUBWA** Kwa meningeyo yote ambayo huna uhakika nayo uliza kwa walimu au viongozi wateule

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Fomu hii ni sharti ijazwe na mwanafunzi na mzazi wa mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na shule hii, na aje nayo wakati anaripoti shuleni

SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi ..... ambaye ni mwanafunzi niliyechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Nkoma Day tokea shule ya msingi ya ..... Nakubali kujiunga na shule. Nitakuwa mwaminifu, mtiifu nitafuata sheria na kuzingatia taratibu zote za shule. Nitatunza mali zote za umma, nitasoma kwa bidii na kufanya kazi za shule kwa uweza wangu wote mpaka nitakapohitimu masomo yangu. Nitaishi kwa amani na kujiheshimu katika mazingira ya shule na jumuiya inayonizunguka.

.....

Sahihi ya Mwanafunzi

SEHEMU YA MZAZI / MLEZI

Mimi ..... mzazi / mlezi wa .....

Naahidi kuwa;-

Mtoto wangu atafika shuleni na vifaa vyote alivyoagizwa na shule kwa wakati uliopangwa

Nitashirikiana na walimu kuhakikisha kuwa mwanangu anaendelea na masomo kipindi chote cha masomo yake

Nitaon taarifa wakati wowote itakapotokea jambo lisilo la kawaida kwa mwanangu

Nitapiga vita suala la utoro ili mwanangu ahudhurie vipindi vyote vya masomo na shughuli mbalimbali za shule.

.....

Sahihi ya mzazi / mlezi

Nakala:-

- Mkaguzi Mkuu wa Kanda
  S.L.P 1025
  TABORA

  Afisa Elimu (M)
  S.L.P 308
  BARIADI – SIMIYU

  Afisa Elimu Sekondari (W)
  S.L.P 308
  BARIADI

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

NKOMA DAY SECONDARY SCHOOL

R QUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF STUDENT EXPECTED TO JOIN FORM ONE 2021

T E MEDICAL OFFICER

.. ..

.. ..

.. ..

N me of student ....

P se examine the above mentioned as to his / her fitness for secondary school education according to the

	ITEM	CONDITION	REMARK
1	Mental condition		
2	Sight		
3	Hearing		
4	Check Tb		
5	Urine		
6	Stool		
7	Nose		
8	Blood HP,HB		
9	Pregnancy test		
10	Anemia		

A y other physical disability not listed that may affect his/ ier studies

.. ..

.. ..

.. ..

Signature .....

Medical Officer .....

Official Stamp .....